# MUHTASARI WA KIKAO CHA DHARURA CHA WAKUU WA IDARA NA VITENGO KILICHOKETI TAREHE 08 FEBRUARI, 2022 KATIKA OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI (W).

**Kumb. SDC/CMT-08/02/2021 - 2022**

**MAHUDHURIO:-**

**WATAALAM WALIOHUDHURIA.**

1. Bi. Lightness S. Msemo - Mkurugenzi Mtendaji (W).
2. Bw. Hamis Mkelle - Afisa Utawala na Utumishi (W)
3. Bi. Mainess Kiluswa - Kaimu Afisa Manunuzi (W)
4. Bw. Vasco Stambuli - Kaimu Mweka Hazina (W)
5. Bw. John Benard - Kaimu Mhandisi wa Ujenzi (W)
6. Bw. Lugano Mwambije - Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii (W)
7. Bi. Lawis Zacharia - Mratibu wa TASAF
8. Bi. Patricia J. Mpewa - Kaimu Afisa Elimu Msingi (W)
9. Bw. Lwitiko Lazaro - Afisa Utumishi
10. Bw. Ambwene Yonah - Afisa Habari (W)
11. Bw. Elias Masangora - Kaimu Mganga Mkuu (W)
12. Bw. Dismas Mwingira - Kaimu Afisa Elimu Sekondari (W)
13. Bi. Fanisia Malesa - Kaimu Mratibu wa UKIMWI (W)
14. Bw. Herbert Mbise - Afisa Sheria (W)
15. Bw. Anderson Mwakyembe- Afisa Usafirishaji (W)
16. Bw. Ipyana Mwakubali - Afisa Mapato
17. Bw. Benedicto Silla - Kaimu Afisa TEHAMA (W)
18. Bw. Marius Kapufi - Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi (W)
19. Bi. Bahati Mgimwa - Afisa Uchaguzi (W)
20. Bw. Mseya Juma - Kaimu Afisa Ufugaji Nyuki (W)
21. Bi. Veronica Mwandiga - Afisa Biashara (W)
22. Bw. Sigfrid Mapunda - Kaimu Mkaguzi wa Ndani (W)
23. Bw. Kabura James Philip - Kaimu Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (W)

**WATAALAM WASIOHUDHURIA.**

1. Bw. Peter Mollel - Mweka Hazina (W) - Kwa Taarifa
2. Bw. Joseph Millinga - Afisa Maendeleo ya Jamii (W) - Kwa Taarifa
3. Bi. Fanikio I. Bitende - Afisa Elimu Sekondari (W) - Kwa Taarifa
4. Bw. Dennis Maghala - Afisa Mifugo na Uvuvi (W) - Kwa Taarifa
5. Bw. Reuben Sanga - Afisa Mipango (W) - Kwa Taarifa
6. Bw. Chande A. Juma - Afisa Ardhi na Maliasili (W) - Kwa Taarifa
7. Bw. Godfrey Maufi - Kaimu Afisa Mazingira na Udhibiti wa Taka Ngumu (W) -Kwa Taarifa
8. Bw. Simon Simbujile - Katibu TSC - Kwa Taarifa

**SEKRETARIETI:**

1. Bw. Aloyce Pius Mwingo - Katibu wa Kamati
2. Bw. Louis L. Kinyonto - Katibu wa Kamati (W)



CamScanner

## MUHTASI NA. SDC/CMT-08/01/02/2021-2022: KUFUNGUA KIKAO.

Kabla ya kufungua Kikao Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili aweze kufungua Kikao.

Baada ya kukaribishwa Mwenyekiti alieleza kuwa, leo tumekutana kwa ajili ya kujadili utaratibu wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, pamoja na kupitia taarifa ya mapendekezo ya ujenzi wa miundominu ya kuboresha huduma za jamii kwa fedha za TASAF III.

Baada ya maelezo hayo Mwenyekiti alifungua Kikao mnamo saa 02:12 asubuhi.

## MUHTASI NA. SDC/CMT-08/02/02/2021-2022: KUSOMA NA KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO.

Agenda zifuatazo zilisomwa na kuthibitishwa kuwa na agenda za Kikao;-

1. Kufundua Kikao.
2. Kusoma na kuthibitisha agenda za Kikao.
3. Utaratibu wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.
4. Mapendekezo ya mradi wa ujenzi wa kisima cha maji na kuongeza matundu ya vyoo eneo la stendi ya Laela kwa fedha za miundombinu kutoka TASAF III.
5. Kufunga Kikao.

## MUHTASI NA. SDC/CMT-08/03/02/2021-2022: UTARATIBU WA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO.

Iliwasilishwa taarifa kuwa, kati ya tarehe 4 Oktoba, 2021 hadi tarehe 27 Januari, 2022 Halmashauri yetu imepokea fedha jumla ya shilingi 4,244,400,000/= kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Miradi iliyopokea fedha ni kama inavyoonekana kwenye jedwali hapo chini;-

| NA. | JINA LA MRADI | AINA YA MRADI | FEDHA POKELEWA |
|---|---|---|---|
| 1. | UJENZI WA VYOO VYA WASH | Ujenzi wa matundu 5 ya vyoo, kichomea taka 1, shimo la kutupia kondo la nyuma, na matenki ya maji Zahanati ya Chitete | 31,487,500/= |
| | | Ujenzi wa matundu 5 ya vyoo, kichomea taka 1, shimo la kutupia kondo la nyuma, na matenki ya maji Zahanati ya Tentula | 31,487,500/= |
| | | Ujenzi wa matundu 5 ya vyoo, kichomea taka 1, shimo la kutupia kondo la nyuma, na matenki ya maji Zahanati ya Kalambazite | 31,487,500/= |
| | | Ujenzi wa matundu 5 ya vyoo, kichomea taka 1, shimo la kutupia kondo la nyuma, na matenki ya maji Zahanati ya Ilemba | 31,487,500/= |
| | | Ujenzi wa matundu 5 ya vyoo, kichomea taka 1, shimo la kutupia kondo la nyuma, na matenki ya maji Zahanati ya Msia | 31,487,500/= |
| | | Ujenzi wa matundu 5 ya vyoo, kichomea taka 1, shimo la kutupia kondo la nyuma, na matenki ya maji Zahanati ya Uzia | 31,487,500/= |
| | | Ujenzi wa matundu 5 ya vyoo, kichomea taka 1, | 31,487,500/= |



CamScanner

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | shimo la kutupia kondo la nyuma, na matenki ya maji Zahanati ya Nkwilo | |
| | | Ujenzi wa matundu 5 ya vyoo, kichomea taka 1, shimo la kutupia kondo la nyuma, na matenki ya maji Zahanati ya Mfinga | 31,487,500/= |
| **Jumla Ndogo** | | | **251,900,000/=** |
| 2 | Mradi wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO - 19 | Ujenzi wa Jengo la Dharura Hospitali ya Wilaya Mtowisa | 300,000,000/= |
| | | Ujenzi wa Nyumba za Watumishi (3 in 1) wa Hospitali ya Wilaya Mtowisa | 90,000,000/= |
| **Jumla Ndogo** | | | **390,000,000/=** |
| 3 | Mradi wa SEQUIP | Ujenzi wa vyumba 8 vya madarasa, jengo 1 la Utawala, Maabara 3, Maktaba 1, Chumba cha TEHAMA, Miundombinu ya Kuvuna Maji, Miundombinu ya kunawia mikono, matundu 20 ya vyoo na tenki 1 Shule ya Sekondari ya Kata ya Nankanga | 470,000,000/= |
| | | Ujenzi wa vyumba 8 vya madarasa, jengo 1 la Utawala, Maabara 3, Maktaba 1, Chumba cha TEHAMA, Miundombinu ya Kuvuna Maji, Miundombinu ya kunawia mikono, matundu 20 ya vyoo na tanki 1 Shule ya Sekondari ya Kata ya Laela | 470,000,000/= |
| **Jumla Ndogo** | | | **940,000,000/=** |
| 4. | Miradi ya Maendeleo kwa fedha za ruzuku kutoka Serikali Kuu | Uendelezaji wa Ujenzi Wa Ofisi ya Mkurugenzi | 1,000,000,000/= |
| | | Ujenzi wa Mochwari na Jengo la Upasuaji na Wodi ya Vidonda ya Wanaume na Wanawake | 800,000,000/= |
| | | Ujenzi wa Nyumba ya Mkurugenzi | 150,000,000/= |
| | | Ujenzi wa Maabara katika Shule 5 za Sekondari | 150,000,000/= |
| | | Ukamilishaji wa maboma 9 ya Shule za Msingi | 112,500,000/= |
| | | Ujenzi wa Zahanati 2 za Ndelema na Kasekela | 150,000,000/= |
| | | Uendelezaji wa Ujenzi wa Kituo cha Afya Mpui | 300,000,000/= |
| **Jumla Ndogo** | | | **2,662,500,000/=** |
| **Jumla Kuu** | | | **4,244,400,000/=** |

Taarifa hiyo ilieleza zaidi kuwa, katika mapokezi hayo ya fedha ipo miradi ambayo mchakato wa utekelezaji umeanza na miradi ambayo mchakato wa utekelezaji haujaanza.

Miradi ambayo mchakato wa utekelezaji umeanza ni kama ifuatavyo;-

**A.** Mradi wa ujenzi wa vyoo vya WASH vyenye thamani ya shilingi 251,900,000/= ambapo Mkandarasi aliyepatikana ni GRIFEDA CO. LTD wa S.L.P 39 Sumbawanga na ameanza kazi.

Mchakato wa utekelezaji wa miradi hiyo uliendelea kutokana na sababu ifuatazo;-

I. Fedha za miradi hiyo zilipokelewa zikiwa na ukomo wa muda na tayari tulikuwa nje ya muda.
II. Utekelezaji wa miradi hiyo kwa jiografia ya Halmashauri yetu na changamoto za hali ya hewa (kipindi cha masika).
III. Upatikanaji wa vifaa kwa wakati.
IV. Kikao ambacho kilitakiwa kupitisha na kuridhia utekelezaji wa miradi hiyo cha mwezi Desemba, 2021, hakikufanyika.



CamScanner

V. Mkandarasi aliyepatikana amekubali kufanya kazi kwa fedha linganifu ya shilingi 31, 480,0000/= ukilinganisha na makadirio halisi ya mradi ambayo ni shilingi 46,747,275/=.

**B.** Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Dharura na Ujenzi wa Nyumba za Watumishi (3 in 1) katika Hospitali ya Wilaya Mtowisa ambapo Mkandarasi aliyepatikana ni Kuyella Interprises Ltd wa S.L.P 2880 Dar Es Salaam - Tanzania.

**C.** Ujenzi wa vyumba 8 vya madarasa, jengo 1 la Utawala, Maabara 3, Maktaba 1, Chumba cha TEHAMA, Miundombinu ya Kuvuna Maji, Miundombinu ya kunawia mikono, matundu 20 ya vyoo na tenki 1 Shule za Sekondari za Kata ya Laela na Nankanga, ambapo, mchakato wa upatikanaji wa mafundi ulifanyika chini ya Kamati za Ujenzi za Kata husika.

Kamati ya Ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Kata ya Laela ilitangaza kazi na kati ya mafundi walioomba mmoja wao alikuwa ni **MAGEREZA** ambaye aliomba kwa njia ya kama "Local Fundi" na kama Mkandarasi. Mapendekezo ya Kamati ni kumtumia Mkandarasi kutokana na sababu zifuatazo;-

I. Wajumbe wa Kamati ni Watumishi wa Shule ya Sekondari Uchile ambao pia wanatakiwa katika utekelezaji wa majukumu yao ya ualimu.
II. Wajumbe wa Kamati ambao si waajiriwa kwa kipindi hiki wamebanwa na shughuli za Kilimo, lakini pia nguvu za wananchi hazitakuwepo kwa kuwa ni msimu wa kilimo na kubanwa na shughuli za Kilimo.
III. Mkandarasi aliomba kwa fedha ndogo ya shilingi 466,000,000/= na baada ya makubaliano amekubali kufanya kazi kwa shilingi 450,000,000/= ukilinganisha na fedha iliyopokelewa, lakini pia ni ndogo kuliko makadirio ya halisi ya ujenzi ambayo ni shilingi 538,000,000/=.
IV. Vyama vya Wafanyakazi vimeomba walimu wasaitumike katika kazi za ujenzi.

Kwa upande wa Shule ya Sekondari ya Kata ya Nankanga, tangazo la utekelezaji kwa kutumia "Force Account" lilitolewa lakini ni kazi nne (4) tu zilizoombwa ambazo ni ujenzi wa vyumba 8 vya madarasa, jengo la Utawala, Jengo la Maabara na Matundu ya Vyoo. Kazi ambazo hazikuombwa ni chumba cha TEHAMA, Maktaba, Miundombinu ya kunawia mikono, Miundombinu ya kuvuna maji pamoja na tenki, na mchakato wa zabuni unaendelea.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi wa Shule ya Kata ya Nankanga amewasilisha maombi ya kutotumia "Force Account" kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo umbali wa eneo la ujenzi wa Shule pamoja na majukumu aliyo nayo ya kusimamia taaluma katika Shule anayoiongoza.

Miradi iliyopokea fedha hivi karibuni ambayo mchakato wa utekelezaji haujaanza ni;-

| NA. | AINA YA MRADI | KIASI | Mapendekezo ya njia ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|
| 1. | Uendelezaji wa Ujenzi Wa Ofisi ya Mkurugenzi | 1,000,000,000/= | Isubiri mkataba unaotekelezwa ukamilike. |
| 2. | Ujenzi wa Mochwari, Jengo la Upasuaji na Wodi ya Vidonda kwa Wanaume na Wanawake katika Hospitali ya Wilaya | 800,000,000/= | Utekelezaji ufanyike kwa njia ya Mkandarasi |



CamScanner

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Mtowisa | | |
| 3. | Ujenzi wa Nyumba ya Mkurugenzi | 150,000,000/= | Utekelezaji ufanyike kwa njia ya Mkandarasi |
| 4. | Ujenzi wa Maabara katika Shule 5 za Sekondari | 150,000,000/= | Utekelezaji ufanyike kwa njia ya "Force Account" na fedha zipelekwe ngazi ya msingi |
| 5. | Ukamilishaji wa maboma 9 ya Shule za Msingi | 112,500,000/= | Utekelezaji ufanyike kwa njia ya "Force Account" na fedha zipelekwe ngazi ya msingi |
| 6. | Ujenzi wa Zahanati 2 za Ndelema na Kasekela | 150,000,000/= | Utekelezaji ufanyike kwa njia ya "Force Account" na fedha zipelekwe ngazi ya msingi |
| 7. | Uendelezaji wa Ujenzi wa Kituo cha Afya Mpui | 300,000,000/= | Utekelezaji ufanyike kwa njia ya Mkandarasi |
| | **Jumla** | **2,662,500,000/=** | |

Aidha, kwa kuzingatia hali halisi ya utekelezaji wa miradi inayoletewa fedha ikiwa na ukomo wa muda, sambamba na ufanisi katika utekelezaji wake, ipo miradi ambayo tumependekeza itekelezwe kwa njia ya Wakandarasi badala ya "Force Account". Sababu kuu za kupendekeza njia ya Wakandarasi ni kama ifuatavyo;-

I. Uhaba wa watumishi wa usimamizi wa miradi kwani Watumishi waliopo ni wachache, ambao pia wana majukumu mengi. Mfano Walimu ambao wana jukumu la kusimamia taaluma katika Shule zao.
II. Kutokana na eneo la utekelezaji wa miradi kuwa nje ya vituo vya kazi, walimu ambao ni wasimamizi wa miradi watashindwa kutekeleza majukumu yao ya msingi.
III. Uzoefu wa miradi iliyopita hasa Miradi ya Madarasa ya UVIKO – 19 unaonesha ushiriki wa Wananchi kutokuwa wa kuridhisha, mfano katika Shule ya Sekondari Lusaka ambapo hakukuwa na nguvu za Wananchi kabisa.
IV. Pia kutakuwa na uhaba wa nguvu kazi ikizingatiwa huu ni msimu wa kilimo.
V. Ugumu katika upatikanaji na usafirishaji wa vifaa vya ujenzi.
VI. Changamoto ya mfumo wa "Force Account" kuhitaji matumizi ya pesa taslimu katika malipo ya mafundi, jambo ambalo linakwamishwa na mfumo wa malipo.
VII. Ukitumia "Force Account" mradi ukiwa chini ya kiwango hasara inakuwa chini ya Mkurugenzi wakati ukitekeleza kwa njia ya Mkandarasi, mradi ukiwa chini ya kiwango hasara ni kwa Mkandarasi na atalazimika kufanya marekebisho kwa gharama zake mwenyewe.
VIII. Ukitumia "Force Account" kunakuwa na hatari kwa Watumishi kupoteza ajira zao na kuingia kwenye migogoro na mashauri ya kinidhamu.
IX. Kutokana na jiografia ya Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga kuwa ngumu katika maeneo mengi, tathmini inaonesha kuwa utekelezaji wa miradi kwa njia ya "Force Account" ni gharama kuliko kutekeleza kwa njia ya Mkandarasi. Mfano, katika ujenzi wa vyoo vya WASH, gharama halisi za utekelezaji ni shilingi 46,747,275/= wakati fedha iliyopokelewa ni shilingi 31,480,000/= ambapo Mkandarasi amekubali kujenga kwa fedha zilizoletwa.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, Wajumbe waiipitia na kuijadili kwa kina, kisha walishauri mapendekezo hayo yawasilishwe katika Kikao cha Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango kwa maamuzi zaidi.



CamScanner

**MUHTASI NA. SDC/CMT-08/04/02/2021-2022: MAPENDEKEZO YA MRADI WA UJENZI WA KISIMA CHA MAJI NA KUONGEZA MATUNDU YA VYOO ENEO LA STENDI YA LAELA KWA FEDHA ZA MIUNDOMBINU KUTOKA TASAF III.**

Iliwasilishwa taarifa kuwa, pamoja na shughuli ya kunusuru Kaya Maskini kwa walengwa kwa kutoa fedha za CCT na kutekeleza miradi ya ajira za muda, TASAF III imeanzisha programu ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu kwa ajili ya kuboresha huduma za jamii kwa sekta za Elimu, Afya na Maji. Katika shughuli hiyo Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga imetengewa fedha kiasi cha shilingi 65,001,100/= kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya miundombinu.

Kutokana na Halmashauri kutengewa fedha hizo, yaliwasilishwa mapendekezo ya kuchimba kisima cha maji na kuongeza matundu ya vyoo eneo la stendi ya Laela, ili kuweza kuboresha huduma ya maji na usafi katika maeneo ya stendi, ili ifikapo tarehe 11/02/2022 andiko liweze kutumwa kwa ajili ya utekelezaji .

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, Wajumbe waliipokea na kuiridhia.

**MUHTASI NA. SDC/CMT-08/05/02/2021-2022: KUFUNGA KIKAO.**

Kabla ya kufunga Kikao Katibu aliwashukuru Wajumbe kwa utulivu waliouonesha, kisha akamkaribisha Mwenyekiti ili aweze kufunga Kikao.

Mwenyekiti alifunga Kikao mnamo saa 04:10 asubuhi.

**UMETHIBITISHWA/HAUKUTHIBITISHWA**

**KATIBU**

**Jina**: Bw. Hamis Mkelle

Sahihi: ……………………………… [signature]

**Tarehe:** 15/03/2022

**MWENYEKITI**

**Jina**: Bi. Lightness Stanley Msemo

Sahihi:…………………………… [signature]

**Tarehe:** 15/03/22



CamScanner